


MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU WA MASIKA MACHI – MEI, 2023



Kielelezo 1: Mwelekeo wa mvua za Machi hadi Mei, 2023

Dondoo muhimu za msimu wa mvua za Masika; Machi - Mei 2023

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa msimu wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi – Mei, 2023, ushauri kwa wadau wa sekta na mamlaka mbalimbali kama vile Kilimo na Usalama wa Chakula, Mifugo na Uvuvi, Utalii na Wanyamapori, Uchukuzi, Mamlaka za miji, Nishati, Maji na Madini, Afya pamoja na Menejimenti za Maafa. Baadhi ya mambo muhimu katika taarifa hii ni: -

- i. Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka isipokuwa maeneo machache ya mikoa ya Dar es salaam, Pwani (ikijumuisha Mafia), kaskazini mwa Morogoro pamoja na kisiwa cha Unguja ambapo mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa.
- ii. Ongezeko la mvua linatarajiwa katika kipindi cha mwezi Mei 2023, hususan katika maeneo ya pwani ya kaskazini.
- iii. Mvua za Masika zinatarajiwa kuanza mwezi Machi, katika maeneo mengi na zinatarajiwa kuisha katika wiki ya nne ya mwezi Mei 2023 katika maeneo mengi ingawa mwendelezo wa mvua za nje ya msimu unatarajiwa mwezi Juni 2023 katika maeneo machache ya ukanda wa pwani ya kaskazini.

Athari zinazotarajiwa:

- i. Mvua chache na zenye mtawanyiko usioridhisha katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani zinaweza kusababisha upungufu wa unyevu kwenye udongo na upatikanaji wa maji kwa ajili ya shughuli za kilimo.
- ii. Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani, unyevu wa udongo kupita kiasi unaweza kujitokeza na hivyo kuathiri ukuaji wa mazao ambayo hayahitaji maji mengi.
- iii. Kwa kuwa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani, viwango vya maji katika mito na mabwawa havitarajiwi kuathirika zaidi.

1. MWENENDO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2022 HADI APRILI, 2023) NA MWELEKEO WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI), 2023

1.1 Mwenendo wa mvua za Msimu (Novemba, 2022 hadi Aprili, 2023)

Mvua za Msimu zilizoanza mwezi Novemba, 2022 katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (mikoa ya Dodoma, Singida, Kigoma, Tabora, Katavi, Rukwa, Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Ruvuma, Lindi, Mtwara na kusini mwa mkoa wa Morogoro) zilinyesha kwa kiwango cha wastani katika kipindi cha Novemba, 2022 hadi Januari, 2023. Mvua hizi zilitawaliwa na vipindi virefu vya ukavu hususan mwezi Novemba, 2022 kwa maeneo ya pwani ya kusini, na kusini mwa mkoa wa Morogoro. Katika kipindi kilichosalia cha msimu (Februari, Machi na Aprili) mvua zinatarajiwa kuendelea kama ilivyotabiriwa mwezi Oktoba, 2022.

1.2 Mwelekeo wa mvua za Masika (Machi hadi Mei), 2023

Msimu wa mvua za Masika ni mahususi kwa maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa katika kipindi cha msimu (kama inavyoelezwa katika kipengele cha 2 cha taarifa hii), kwa ujumla mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga pamoja kisiwa cha Pemba katika msimu wa mvua za Masika, 2023. Hata hivyo, mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo ya mikoa ya Dar es Salaam, Pwani (ikiwemo visiwa vya Mafia), kaskazini mwa mkoa wa Morogoro na kisiwa cha Unguja. Ongezeko la mvua linatarajiwa mwezi Mei, 2023 katika maeneo hayo. Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

i. Kanda ya Ziwa Victoria: (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kakonko na Kibondo):

Mvua za Masika zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani katika maeneo mengi ya ukanda wa Ziwa Victoria pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. Mvua hizo zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi, 2023 na zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Mei, 2023.


ii. Ukanda wa Pwani ya Kaskazini: (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mkoa wa Pwani (ikijumuisha kisiwa cha Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):

Mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani (ikiwemo visiwa vya Mafia), kaskazini mwa mkoa wa Morogoro na kisiwa cha Unguja.

Aidha, mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa kunyesha katika maeneo ya mkoa wa Tanga pamoja kisiwa cha Pemba. Mvua hizo zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Machi, 2023 na kuisha Juni, 2023.

iii. Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki: (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):

Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani na zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Machi, 2023. Mvua hizo zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2023.



Kielelezo 2: *Kushoto: Mwelekeo wa mvua za Masika (Machi –Mei), 2023 na Kulia: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za Masika (1991-2020).*

Angalizo 1: *Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani.*

Angalizo 2: *Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia taarifa za utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi na tahadhari kama zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).*

2. MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kati la bahari ya Pasifiki. Vilevile, joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo kubwa la kitropiki la bahari ya Hindi. Kwa upande mwingine, joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki. Hali hiyo inatarajiwa kudhoofisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, kaskazini mwa mkoa wa Kigoma, nyanda za juu kaskazini-mashariki na pwani ya kaskazini.

Vilevile, joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi hususan katika kipindi cha kuelekea mwishoni mwa msimu. Hali hii inatarajiwa kusababisha unyevuanga kutoka baharini kuingia katika eneo la mashariki mwa nchi hasa katika kipindi cha mwezi Mei 2023.

3. ATHARI NA USHAURI

Athari za kisékta na ushauri uliotolewa hapa chini umeandaliwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa kushirikiana na wataalam wa sekta husika katika mkutano wa wadau wa hali ya hewa uliofanyika tarehe 20 Februari, 2023. Wadau wa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii wanashauriwa kupanga na kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia taarifa mahususi za hali ya hewa zinazotolewa na TMA.

a) Kilimo na Usalama wa Chakula

Shughuli za kilimo zinatarajiwa kuendelea kama ilivyo kawaida. Hata hivyo, kwa baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kupata mvua chache zenye mtawanyiko hafifu, yanaweza kukumbwa na upungufu wa unyevu wa udongo na upatikanaji wa maji kwa shughuli za kilimo na hivyo kuathiri uzalishaji wa mazao hasa katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa Ziwa Victoria. Hata hivyo, vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa baadhi ya mazao yasiyohitaji maji mengi, kama vile mahindi na mazao jamii ya mikunde, hususani kwa mikoa ya pwani ya kaskazini inayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani.

Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati, kutumia mbinu bora na teknolojia za kuzuia maji kutuama shambani, mmomonyoko na upotevu wa rutuba, na kuchagua mbegu na mazao sahihi kwa ajili ya msimu huu wa Masika. Aidha, inashauriwa kuimarisha miundombinu ya kilimo pamoja na uvunaji maji ya mvua na kudhibiti visumbufu vya mimea ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

b) Mifugo na Uvuvi

Upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo na chakula cha samaki unatarajiwa kuwepo kama ilivyo kawaida. Hata hivyo, kwa baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kupata mvua chache yanaweza kuathirika kiasi kutokana na upatikanaji hafifu wa maji, malisho na chakula cha mifugo na samaki. Hii inaweza kupelekea athari katika uzalishaji wa bidhaa za mifugo na zile za uvuvi katika maeneo machache yanayoweza kupata mvua chini ya wastani. Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji kama vile malisho ya mzunguko ili kutunza malisho na kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadae. Jamii inashauriwa kuweka mipango mizuri ya matumizi bora ya maji na malisho. Vilevile, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kufuatilia mirejeo ya tabiri za hali ya hewa na ushauri kutoka kwa maafisa ugani ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza. Kwa upande mwingine, katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani, wafugaji na wavuvi wanatarajiwa kufaidika na upatikanaji wa malisho na chakula cha samaki. Wafugaji na wavuvi wanashauriwa kufuatilia tabiri za hali ya hewa na ushauri kutoka kwa maafisa ugani ili kutumia fursa hii kuongeza tija katika msimu huu wa mvua.

c) Utalii, Maliasili na Wanyamapori

Hali ya malisho na maji kwa ajili ya wanyamapori katika mbuga na hifadhi inatarajiwa kuwa ya kawaida. Hata hivyo, upungufu wa mvua unaotarajiwa katika baadhi ya maeneo unaweza kusababisha upungufu wa maji na malisho kwa wanyamapori na kupelekea wanyamapori kuhama kwa ajili ya kutafuta maji na malisho, hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani na pia inaweza kupelekea magonjwa ya wanyamapori kusambaa kwa wanyama wanaofugwa na binadamu kutokana na wanyamapori kuingia katika makazi ya jamii zinazozunguka hifadhi na mbuga.

Mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu mbalimbali katika hifadhi za wanyamapori na kujenga uelewa kwa jamii ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kutokana na hali ya mvua inayotarajiwa. Hivyo basi, jamii inashauriwa kutoa taarifa kwa mamlaka husika iwapo wanyamapori wataingia katika makazi au maeneo mbalimbali ya watu.

d) Usafiri na Usafirishaji

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani, shughuli za usafiri na usafirishaji zinatarajiwa kuwa za kawaida. Matukio ya hali mbaya ya hewa yanaweza kuharibu miundombinu ya barabara na reli, ongezeko la ajali barabarani katika usafiri wa nchi kavu; kuchelewa au kusitishwa kwa safari za ndege, mawasiliano hafifu angani na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji katika usafiri wa anga. Hata hivyo, sekta ya usafirishaji, hususan ya usafiri wa nchi kavu, inatarajiwa kunufaika katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Wadau wa sekta hii wanashauriwa kuchukua tahadhari ya matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa ambayo yanaweza kuleta uharibifu wa miundombinu ya usafirishaji.

e) Nishati, Maji na Madini

Upatikanaji wa maji unatarajiwa kuimarika, hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Kina cha maji katika mabwawa na mito kinatarajiwa kuongezeka. Hata hivyo, athari katika miundombinu ya rasilimali maji inaweza kujitokeza. Shughuli za uchimaji madini hususan katika migodi midogomidogo zifanyike kwa kuzingatia tahadhari zinazotolewa kwani ongezeko la maji katika udongo linaweza kusababisha maporomoko ya ardhi. Aidha, maeneo ambayo mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa, kina cha maji katika mabwawa kinatarajiwa kupungua, hivyo matumizi sahihi ya maji kwa ajili ya umwagiliaji, majumbani pamoja na kuendesha mitambo ya umeme yanashauriwa.

Wadau wanashauriwa kuzingatia matumizi endelevu na uhifadhi wa rasilimali maji katika shughuli za uchakataji wa madini, uzalishaji wa umeme, matumizi ya viwandani na majumbani. Hali kadhalika, mamlaka husika zinashauriwa kuweka mipango madhubuti ya uzalishaji wa nishati ya umeme kutoka vyanzo vingine tofauti na maji kama vile nishati ya jua, upepo na gesi.

f) Mamlaka za Miji

Katika maeneo yanayotarajia kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani, mamlaka za miji zinashauriwa kuhifadhi maji yatakayopatikana, kuandaa na kujenga mifumo ya kuvuna maji ya mvua.

Kwa upande mwingine, katika maeneo yanayotarajia mvua za wastani hadi juu ya wastani, mvua zinatarajiwa kusababisha kutuama kwa maji na mafuriko, hivyo kusababisha uharibifu wa miundombinu, upotevu wa mali. Mamlaka za miji zinashauriwa kuboresha na kutunza mifumo ya mifereji ya maji ili kupunguza athari za kutuama kwa maji na mafuriko na kutoa uelewa kwa umma juu ya hatua stahiki zinazofaa kuchukuliwa.

g) Sekta ya Afya

Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinazotarajiwa zinaweza kuathiri upatikanaji wa maji safi na salama ambapo inaweza kupelekea mlipuko ya magonjwa. Mamlaka za afya zinashauriwa kuchukua hatua stahiki kupunguza athari zinazoweza kujitokeza, ikiwa ni pamoja na kuhimiza wananchi kutibu maji kabla ya kutumia pamoja na kunywa maji safi na salama. Pia, jamii inashauriwa kuchukua hatua kwa kuhakikisha usafi wa mazingira yanayowazunguka, kuharibu mazalia ya mbu na kudumisha usafi kwa ujumla.

Katika maeneo ambayo mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa, maji yaliyotuma juu ya ardhi na utiririshaji wa maji taka usiodhibitiwa unaweza kusababisha uchafuzi wa maji na kusababisha mlipuko wa magonjwa kama vile magonjwa yatokanayo na wadudu dhurifu na magonjwa yanayoenezwa na maji. Mamlaka husika zinashauriwa kuhakikisha uwepo wa dawa za kutosha katika vituo vya afya kwa kuzingatia uwezekano wa uharibifu wa miundombinu ya usafirishaji.

h) Sekta Binafsi

Wakulima wa mashamba makubwa wanaweza kuathirika kutokana na uchache wa mvua wenye mtawanyiko usioridhisha hususan kwa maeneo yanayotarajia kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Hali hii itasababisha kuwepo kwa matumizi makubwa ya nishati ya kumwagilia na kuhifadhi mazao tete na bidhaa. Hali kadhalika, uchache na mtawanyiko wa mvua usioridhisha unaweza kusababisha kuathirika kwa ubora wa miti ya nguzo na mbao.

Wadau wa Sekta binafsi wanashauriwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali ikiwemo wataalam wa hali ya hewa ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza. Taasisi za Benki na Bima zinashauriwa kuandaa na kutoa huduma mahususi kwa wadau ili kujenga ustahimilivu katika biashara.

i) Menejimenti za Maafa

Upungufu wa mvua unaoweza kujitokeza unaweza kusababisha upungufu wa unyevu katika udongo, chakula, malisho ya mifugo na maji. Aidha, uharibifu wa miundombinu, upotevu wa mali na madhara kwa binadamu vinaweza kutokea kutokana na vipindi vifupi vya mvua kubwa vinavyoweza kujitokeza. Hivyo, mamlaka husika na kamati za usimamizi wa maafa katika ngazi ya mkoa, wilaya, kata na vijiji zinashauriwa kuzifuatilia taarifa za tahadhari na

kushirikiana na kuchukua hatua za kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na maafa yanayoweza kujitokeza.

j) Vyombo vya habari

Vyombo vya habari vinashauriwa kupata utabiri, kufuatilia na kusambaza taarifa na tahadhari za hali ya hewa pamoja na zile zilizo huishwa na Mamlaka. Jamii inasisitizwa kutumia taarifa mahsus za hali ya hewa kwa matumizi ya kissekta. Vyombo vya habari vinashauriwa kutafuta na kutumia ushauri wa kissekta kutoka sekta husika wakati wa kutayarisha na kutoa taarifa mtambuka za hali ya hewa kwa jamii. Aidha, vyombo vya habari vinashauriwa kuandaa na kusambaza makala za kitaalamu kwa kutumia lugha nyepesi kwa lengo la kuhabarisha jamii juu ya matumizi sahihi ya utabiri wa hali ya hewa kwa kutumia radio na televisheni za kitaifa na mahalia.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wote wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, mamlaka za wanyamapori, wasafirishaji, mamlaka za maji na afya kuendelea kutafuta, kupata na kuzingatia ushauri wa wataalam katika sekta husika.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa mirejesho ya mwelekeo wa mvua nchini kadri inavyohitajika. Aidha, wadau wanashauriwa kuwasiliana na Mamlaka ili kupata taarifa mahsusi za utabiri wa msimu ili kukidhi mahitaji maalum katika sekta zao.

Imetolewa: 22 Februari, 2023

Na: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania